



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 29 Mei, 2021.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka 2021/2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka 2021/2022.

II. **MASWALI:**

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

217. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa jitihada zake za kupambana na vitendo vya rushwa nchini. Licha ya Serikali kuweka wakaguzi wa ndani katika kila ofisi bado kulikuwa na mianya ya upotevu wa fedha nyingi, mpaka Serikali ilipoanzisha Sheria ya ZAECA ya mwaka 2012.

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wakaguzi wazembe waliosababisha upotevu wa fedha nydingi za Serikali.
- (b) Je, Serikali haioni haja ya kupunguza vyombo hivyo vya ukaguzi na kubakisha kati ya ZAECA au CAG ili kupunguza urasimu wa utendaji kazi wa kupambana na vitendo vya rushwa.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

133. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wafanyabiashara wadogo wadogo waliokuwepo katika eneo la kituo cha daladala cha Kijangwani tayari wamehamishwa na kuendelea na shughuli zao katika eneo la Kibandamaiti.

- (a) Je, ni lini kituo cha daladala cha Kijangwani kitatumika kwa ajili ya shughuli yake iliyokusudiwa.
- (b) Kwa kuwa sehemu ya Mwembeladu kuna kituo ambacho kimezidiwa na gari za abiria pamoja na teksi, Je, Serikali haioni haja ya gari hizo kuhamishiwa katika kituo hicho cha Kijangwani.

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

184. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika malengo ya Bajeti ya mwaka 2020/2021 Serikali ya Zanzibar ilikusudia kuanza ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Abdalla Mzee.

- (a) Je, Wizara yako inalifahamu lengo hilo.
- (b) Je, ujenzi huo umefikia wapi mpaka sasa.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

145. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara zetu nyingi zilizojengwa ziko ambazo hazijamaliziwa kujengwa katika maeneo ya maporomoko ya maji milimani, jambo ambalo hupelekea kukatika katikati kwa barabara hizo wakati wa msimu wa mvua.

Je, ni lini Serikali itazikamilisha barabara hizo ili kuepusha tatizo hilo.

216. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi :

Serikali imekuwa ikichukuwa jitihada kubwa za kujenga na kuzifanya matengenezo barabara mbali mbali Unguja na Pemba. Kwa upande wa Jimbo la Pandani kuna barabara fupi ya kutoka Ambasha-Mitukawani ujenzi wa barabara hiyo umekwama hadi leo licha ya malighafi za utengenezaji barabara hiyo kuwepo kwenye eneo hilo.

(a) Serikali ituambie ni kwanini hadi leo barabara hiyo haijakamilika.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuikamilisha barabara hiyo na kwa kiwango gani.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,
29 Mei, 2021.

(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA